

## **Mchango wa Fonolojia katika Kuuelewa Ushairi Andishi wa Kiswahili**

**Aginiwe N. Sanga**  
**Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Dodoma**

vogosivopala@gmail.com

### **Ikisiri**

Wataalamu mbalimbali wanabainisha kuwa kueleweka kwa ushairi kunategemea sana kuielewa fani kwa kuwa ndio nyenzo iwasilishayo maudhui. Kwa mintarafu hii, hatuna budi kuvielewa vipengele mbalimbali vya kifani vilivyotumika katika mashairi husika kama vile tamathali za semi, picha na ishara, muundo, mtindo na wahusika (Wamitila, 2004 na Mulokozi, 2017). Hata hivyo, wataalamu wengine wanabainisha wazi kuwa kazi yoyote ya fasihi, ukiwamo ushairi, hutumia lugha kuwasilisha maudhui hayo. Hivyo, ili kuyaelewa maudhui yanayowasilishwa na mashairi, uchambuzi wa lugha iliyotumika ni suala muhimu sana (Njogu na Chimera, 2008). Aidha, ifahamike kuwa kueleweka kwa mashairi kunategemea sana kueleweka kwa vipengele mbalimbali vya kisarafu (kama vile vya kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki) vilivyotumika katika shairi husika. Kutokana na hilo, makala hii inafafanua mchango wa fonolojia katika kueleweka kwa ushairi. Ili kufanya hivyo, makala hii imechambua vipengele mbalimbali vya kifonolojia vilivyomo katika vitabu viwili, Mashairi ya Saadani (1972) na Malenga wa Bara (1976). Utafiti uliozalisha makala hii ulikuwa wa maktabani, na uwandani. Aidha, data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi matini na ushuhudiaji. Uchambuzi na uwasilishaji wa data ulizingatia Nadharia ya Umuundo. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa fonolojia ina mchango mkubwa katika kuuelewa ushairi kupitia vipengele vya mpangilio wa fonimu na uradidi wake katika ushairi, uradidi wa silabi, wizani, mkazo na kiimbo.

**Dhana za Msingi:** Fonolojia, Ushairi, fonolojia vipande na fonolojia arudhi

## **Utangulizi**

Wazo la msingi la wanaumuundo katika fasihi ni kwamba kazi za fasihi ni muundo unaojumuisha vipengele mbalimbali vinavyohusiana. Umuhimu na maana ya kila kipengele hujulikana wakati kipengele hicho kinahusiana na vipengele vingine katika kazi za fasihi. Kipengele kimoja kikiangaliwa peke yake hakina maana (Culler, 1975 na Selden, 1989). Ushairi, kama mmojawapo wa miundo hiyo, umeundwa kwa vipengele mbalimbali vya fani na maudhui. Hivyo, kuuelewa ushairi kunategemea sana kuielewa fani kwa kuwa ndio nyenzo iwasilishayo maudhui. Hii ina maana kuwa, ili kuyaelewa maudhui yanayowasilishwa na msanii yeyote wa kifasihi, hatuna budi kuvielewa vipengele mbalimbali vya kifani vilivyotumika katika kazi husika ya fasihi. Vipengele vya kifani ambavyo vimekuwa vikitajwa sana ni pamoja na tamathali za semi, picha na ishara, muundo, mtindo na wahusika (Wamitila, 2004 na Mulokozi, 2017). Kutokana na mkabala huu wa mawazo, kuna wataalamu na wahakiki mbalimbali ambao wamekuwa wakichambua vipengele vya kifani katika tanzu mbalimbali, ukiwamo ushairi, ili kuwezesha kueleweka kwa tanzu husika. Miongoni mwa wataalamu hao ni Wamitila (2008), Njogu na Chimerah (2008) na Mulokozi (2017). Hawa wamechambua vipengele vya kifani katika riwaya, tamthiliya, hadithi fupi, na ushairi. Kwa ujumla, kinachoonekana katika mkabala huu wa kiuchambuzi ni kuangalia vipengele mbalimbali vya kifani vinavyojenga kazi husika ya fasihi ili kuwasilisha maudhui yake. Hata hivyo, ingawa lugha ndio nyenzo kuu inayotumiwa katika kazi ya fasihi kuwasilisha maudhui, tunaona kuwa haichambuliwi vya kutosha, hususani vipengele mbalimbali vya kisarufi katika lugha vinavyojumuisha fonolojia, mofolojia, sintaksia, na semantiki.

Kwa upande mwingine, kuna wataalamu wengine wanaobainisha kuwa kazi yoyote ya fasihi, ukiwamo ushairi, hutumia lugha kuwasilisha maudhui hayo (Wamitila, 2004; Njogu na Chimerah, 2008 na Senkoro, 2011). Hivyo, ili kuyaelewa maudhui yanayowasilishwa na kazi yoyote ile ya fasihi, uchambuzi wa lugha iliyotumika ni suala muhimu sana. Hii inamaanisha kuwa kueleweka kwa mashairi kunategemea kueleweka kwa vipengele mbalimbali vya kisarufi vilivyotumika katika kazi husika ya fasihi. Hivyo, yanapochambuliwa matumizi ya lugha (kama kipengele kimojawapo cha fani), ni muhimu pia kuchambua sarufi husika ya lugha na mchango wake katika maudhui badala ya kuishia tu kuchambua lugha za picha, ishara na nyingine. Kutokana na hilo, na kwa kuwa si rahisi kwa makala moja kama hii kuchambua vipengele vyote vya kisarufi vya kazi ya fasihi, makala hii inachambua mchango wa fonolojia katika kueleweka kwa ushairi.

Uchambuzi unaonesha kuwa ushairi, kama zilivyo kazi nyingine za fasihi, hutumia vipengele mbalimbali vya kifonolojia ili kuwasilisha maudhui yake. Aidha, kwa kuwa isingekuwa rahisi kwa makala kama hii kuchambua vipengele vyote, tumbainisha na kuvifafanua vipengele vichache vya kifonolojia. Navyo ni mpangilio na uradidi wa fonimu, silabi, wizani, mkazo, na kiimbo. Vipengele hivi vimeteuliwa kutokana na wataalamu mbalimbali kubainisha kuwa vina mchango mkubwa sana katika kueleweka kwa ushairi (Msokile, 1993; Wamitila, 2010; Senkoro, 2011 na Mulokozi, 2017). Aidha, hivi ni vipengele vya kisauti na sauti ni nyenzo muhimu katika utungo wa kishairi. Hivyo, kwa jumla, tumechambua vipengele hivi vya kifonolojia kwa kuzingatia jinsi vinavyotupatia taarifa za kiisimu kuhusu ushairi. Katika uchambuzi tumezingatia fonolojia vipande sauti na fonolojia vipamba sauti (kiprosodi). Fonolojia vipande sauti inahusika na

fonimu pamoja na alofoni zake. Fonolojia vipamba sauti inahusu sifa bandikizi za vitamkwa vikubwa kuliko fonimu ambavyo husaidia kupambanua maana katika maneno au tungo (Sanga na Philipo, 2017). Katika makala hii, tumefafanua namna kiimbo na mkazo vinavyoweza kuathiri maudhui yanayowasilishwa na mashairi. Msingi wa ushairi haupo katika upangaji mzuri wa maneno unaokidhi vigezo vya usanifu wa lugha husika, bali upo katika nguvu ya matamshi yanayonasibishwa na utamaduni wa lugha na muktadha wa kijamii.

### **Kiunzi cha Nadharia**

Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Umuundo. Hii ni nadharia iliyojikita katika elimu kuhusu miundo. Wazo la msingi la nadharia hii ni kuwa mahusiano ya miundo ndiyo hutupatia maana. Kupitia nadharia hii, kazi za fasihi zimeundwa na vipengele mbalimbali vya kifani vilivyo katika mfumo, ambavyo vinashirikiana na kutegemeana katika kuwasilisha maudhui ya kazi husika ya fasihi (Wafula na Njogu, 2007). Nadharia hii iliyoasisiwa na mwanazuoni wa Kiswidi aitwaye Ferdinand De Saussure na baadaye kutumika katika fasihi, inabainisha wazi kuwa kazi ya fasihi, ukiwamo ushairi, inakamilika tu ikiwa kuna vipengele vikuu viwili, maudhui na fani. Aidha, vipengele hivyo vikuu vina vipengele vingine vidogovidogo vinavyotegemeana na kujengana. Maudhui yana vipengele kama vile dhamira, falsafa, migogoro, suluhisho, na mafunzo wakati fani ina vipengele kama vile matumizi ya lugha, muundo, mtindo, wahusika na mandhari. Vipengele vya maudhui huwasilishwa na vipengele mbalimbali vya kifani vilivyotumika katika kazi husika (Samwel, 2012). Hivyo, nadharia hii imetusaidia sana kubainisha vipengele vya kifani, hasa vya kifonolojia, vilivyotumika katika mashairi teule na kufafanua jinsi vilivyojenga vipengele mbalimbali vya kimaudhui vya mashairi husika.

### **Methodolojia**

Utafiti uliozalisha makala hii, ni wa maktabani, na uwandani, ambapo ulifanyika katika maktaba ya Ndaki ya Insia na Sayansi za Jamii ya Chuo Kikuu cha Dodoma. Katika maktaba hiyo, maandiko mbalimbali kuhusu mada iliyoshughulikiwa yalipitiwa. Pia, mtafiti alishuhudia matamshi ya baadhi ya fonimu kupitia vipindi mbalimbali katika redio FM za jiji la Dodoma. Vipengele vya kifonolojia vimechambuliwa kupitia kitabu cha *Mashairi ya Saadani* cha Saadani A. Kandoro na *Malenga wa Bara* (1972) cha Kulikoyela K. Kahigi pamoja na Mugyabuso M. Mulokozi. Mashairi yaliyomo katika kitabu cha *Mashairi ya Saadani* (1976) ni ya kimapokeo, yaani yametungwa kwa kuzingatia kanuni za utunzi za wanamapokeo kama vile kanuni za urari wa mizani na vina. Kitabu hicho kimeteuliwa kama sampuli kuwakilisha mashairi ya kimapokeo. Aidha, katika mashairi hayo kuna mdhihiriko bayana wa vipengele vya kifonolojia na kuna ukwasi wa fani iliyoepa. Mwandishi Kandoro alikuwa mwanasiasa, katika kitabu chake cha *Mashairi ya Saadani* yapo mashairi yanayozungumzia harakati za ukombozi wa Tanzania na Afrika kwa ujumla, yapo yanayosherehekea uhuru, na ujenzi wa jamii mpya. Mashairi yaliyomo katika kitabu cha *Malenga wa Bara* ni mchanganyiko wa mashairi ya kimapokeo na ya kisasa. Mulokozi na Kahigi katika *Malenga wa Bara* wametunga mashairi yaliyosheheni uradidi wa vipashio vya kifonolojia na hii ndio sababu ya kukitumia kitabu hiki katika uchambuzi. Aidha, *Malenga wa Bara* kinasawiri maisha ya Watanzania baada ya uhuru. Humo yamejadiliwa maudhui yanayohusiana na haki, rushwa, matabaka, mapenzi na ukombozi kwa wanyonge. Mashairi yaliyomo katika vitabu vyote viwili yamekuwa kiwakilishi kizuri katika uchambuzi wa vipengele vya kifonolojia katika

ushairi wa Kiswahili. Hivyo, data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi matini na ushuhudiaji. Jumla ya mashairi kumi yalichambuliwa katika utafiti ambapo mashairi sita yametoka katika Mashairi ya Saadani na manne katika Malenga wa Bara. Aidha, kupitia watangazaji wa vipindi mbalimbali katika redio FM za Dodoma tulishuhudia utamkaji wa sauti mbalimbali zilizoshughulikiwa na utafiti. Uchambuzi na uwasilishaji wa data umezingatia mkabala wa kitaamuli na kuongozwa na Nadharia ya Umuundo. Mkabala wa kitaamuli ulitumika kwa kuwa data zilikusanywa na kuchambuliwa kwa kujigeza katika mitazamo, fikra na maoni ya wahojiwa (Sanga, 2018).

### **Matokeo ya Utafiti**

Ili kubainisha mchango wa fonimu katika kueleweka kwa mashairi teule, makala hii imejikita katika ufafanuzi wa vipengele vya kifonolojia vya: Mpangilio na uradidi wa fonimu, mpangilio na uradidi wa silabi (vina), wizani, kiimbo na mkazo. Ufuatao ni ufafanuzi wa mchango wa vipengele hivyo kwa kudondoa mifano kutoka katika mashairi teule huku ikishadidiwa na hoja za wataalamu mbalimbali:

### **Mchango wa mpangilio na uradidi wa fonimu**

Wataalamu wanakubaliana kuwa fonimu za lugha ndizo msingi wa ushairi. Mshairi huzipanga kwa pamoja fonimu irabu, konsonanti na viyeyusho kwa namna ambayo zitaleta mvuto na maana kwa msomaji. Wanaendelea kubainisha kuwa ushairi hutumia lugha ya mkato, na hivyo bila kuwapo kwa mvuto katika utungo huo, ushairi ungekuwa ni utungo unaokifu. Wanaeleza kuwa mvuto katika ushairi hutokana na marudiorudio ya fonimu irabu, konsonanti na viyeyusho (Wamitila, 2002).

Bahadorj na Mohammadjalil (2012) wanaeleza kuwa, katika uchambuzi wowote wa kifasihi, hoja tatu muhimu kuhusu fonimu lazima zizingatiwe: Mosi, fonimu huvuta umakini pale inaporudiwarudiwa na kuonekana kwa wazi. Pili, kuchunguza nafasi ilipokusudiwa fonimu kuwapo katika maneno na katika sentensi. Tatu, fonimu itakuwa na athari kama itajitokeza mara nyingi katika kipande cha mshororo na, wakati mwingine, kurudiwa kwa fonimu husaidia katika kuleta dhana ya upya wa maana katika maneno. Wataalamu hawa wanakwenda mbele zaidi kwa kuainisha sifa za makundi mbalimbali ya fonimu kama ifuatavyo: Irabu /a, ε, i, o, u/ hizi ni sauti zenye sifa ya msikiko; vipasuo /p, b, t, d, k, g/ ni sauti ngumu, ni sauti zinazorejelea uasili na uhalisi, ugumu na ukavu, mwendo wa kishindo na nguvu, ni sauti zenye msikiko wa ukali na ukatili. Pia, sauti za vipasuo hutumika kama kejeli kwa hali ya uzembe na majuto. Nazo kontinuanti, ni sauti zenye uendelezi. Mfano wa sauti zinazohusishwa na ukontinuanti ni vikwamizi kama vile /f, v, s, z, ʃ/. Kontinuanti, katika ushairi, zinatumika hasa kwa maneno yanayotokana na mwigo wa sauti, yaani onomatopea, na huweza kutumika katika ushairi pamoja na sauti nyingine ili kukidhi malengo yanayotarajiwa na mwandishi. Navyo, ving'ong'o ni kundi la sauti zinazotumia mkondo hewa wa chemba ya pua na katika Kiswahili kuna sauti tano za ving'ong'o: /m, n, ŋ, ɲ, ɳ/. Katika ushairi, aghalabu sauti hizi zitumiwapo huambatana na hisia za kutoridhishwa au kutofurahishwa na jambo. Vilainisho /r, l/, kwa upande mwingine, ni sauti ambazo huambatana na hali ya kumimina kitu kama vile maji na vimiminika vingine. Vikwamizi /f, v, s, z, ʃ, θ, ð, h, x, γ/ ni sauti ambazo hutumiwa na washairi, hasa katika kumithilisha hali ya wororo, ukimya, mvumo wa upepo, hisia za majuto, wivu, laana, woga, chungu na kubezwa au kutwezwa. Vipasuo kwamizi /tʃ, dʒ/ ni sauti ambazo hutumika hasa kurejelea mwendo wa harakaharaka na

kimyakimya, kueleza hisia za maumivu na manung'uniko. Navyo, viyeyusho /j, w/ huhusishwa na hali ya kudumu au kutoisha kwa jambo. Ufafanuzi zaidi wa makundi haya ya sauti na udhihirikaji wake katika ushairi wa Kiswahili umeoneshwa katika vipengele kadhaa wa makala hii hapa chini.

Kutokana na ufafanuzi wa makundi hayo ya sauti za Kiswahili na dhima zake katika kazi za fasihi, wataalamu wanakubaliana kuwa fonimu katika ushairi zina dhima za kuwasilisha, kubeba au kueleza dhana, kusisitiza maudhui, kuwasilisha hisia, kuleta umuziki na kuleta muunganiko wa kiuajumi. Hivyo, hoja ya msingi hapa ni kwamba, mshairi huteua sauti kulingana na picha pamoja na hisia zinazomjia akilini mwake. Kutokana na hilo, huchagua sauti zenye uwezo wa kuwasilisha picha na hisia alizonazo kichwani ili ziwaathiri na hadhira pia bila kutumia njia ya maelezo yaani kwa njia ya mkato. Hoja ya kuwapo kwa vipande sauti akilini mwa wamilisi wa lugha vyenye maana ndani ya mfumo lugha wa jamii, ilishadidiwa pia na wataalamu wakongwe wa isimu kama vile Jan Baudouin De Courtenay, Ferdinand De Saussure na Leonard Bloomfield (Massamba, 2010).

Utafiti ulioizaa makala hii una matokeo yanayokaribiana na ya wataalamu wengine. Imebainika kuwa washairi huteua fonimu za kuzitumia katika mashairi yao ili kuwasilisha maudhui. Aidha, imebainika kuwa uradidi wa fonimu mbalimbali katika mashairi una dhima ya kuwasilisha maudhui kusudiwa. Hili linabainika wazi katika *Mashairi ya Saadani* kwenye shairi lililopewa jina 'Ondoka Nchini Mwetu' (kur. 141-142) kama inavyobainika katika ubeti ufuatao:



Ondoka tukilingana, tuje kwenu uje kwetu,  
Mikono tukipeana, huru Afrika yetu,  
Si vyema kupunjana, mle vyenu tule vyetu,  
Ondoka Nchini mwetu, mwishoni mwa mwaka huu.

Shairi hili lina uradidi wa sauti konsonanti /k/ na uradidi wa sauti konsonanti /t/ kama inavyooneshwa katika ubeti ulionukuliwa hapo juu. Mpangilio wa sauti hizo ni wa kimakusudi. Sauti hizo zipo katika kundi la vipasuo, ambazo ni sauti zenye msikiko wa kulipuka. Aidha, kama inavyofafanuliwa na Bahadorj na Mohammadjalil (khj), hizi ni sauti zinazoashiria ugumu, nguvu, ukali, ukatili, ukavu, na kishindo. Mwandishi Kandoro alitunga shairi hili kipindi cha kupigania uhuru wa Tanganyika kwa lengo la kupinga utawala wa Waingereza. Toni ya shairi hili ni ya ukali ikiwakilishwa na sauti za vipasuo tulizozitaja hapo juu. Senkoro (1988) anashadidia suala hili kwa kueleza kuwa Kandoro ni miongoni mwa washairi katika kipindi cha ukoloni ambao hawakuwa na chembe ya uoga. Kandoro aliandika mashairi yaliyoikashifu serikali ya kikoloni wakati serikali hiyo bado ikiwa imeshika hatamu. Senkoro anabainisha wazi kuwa shairi la ‘Kwetu ni Kwao kwa Nini?’ lina msikiko wa sauti ya ukali na yenye hasira akionesha hasira yake kwa wakoloni. Kutokana na ufafanuzi huu inahalisika kuwa fonimu anazoteua mtunzi wa shairi wakati wa utunzi huwa mwanngwi wa kile kilichomo akilini mwa mtunzi.

Pia, katika maneno tangulizi ya ufafanuzi kuhusu shairi la ‘Usiku Ukikomaa Karibu Kupambazuka,’ Kandoro anaeleza kuwa alitunga shairi hilo ili kufundisha uvumilivu katika mambo. Alitunga shairi hilo liwasaidie wasomaji kuwa na moyo mgumu wanapopitia mambo magumu. Hili linabainika pia katika beti zake kama inavyonukuliwa katika (kur. 78 - 79):

**Kipigo ukipigika, mfano wa kulemaa,  
Ndipo juto hukufika, wakati wachuchumaa,  
Na kupona kutafika, usiondoe tamaa,  
Usiku ukikomaa, karibu kupambazuka.**

Mwana faham hakika, shika yangu kakomaa,  
Shika yangu bila shaka, na ndipo utakomaa,  
**Karibu kupambazuka, usiku ukikomaa,  
Usiku ukikomaa, karibu kupambazuka.**

Uchambuzi wa beti hizi umebainisha kuwapo kwa marudiorudio ya fonimu konsonanti za vipasuo ambazo ni pamoja na /p, b, t, d, k, g/. Kama ilivyofafanuliwa na Bahadorj na Mohammadjalil (khj), vipasuo ni sauti zinazoashiria hali kama za ugumu, uasili, uhalisi na ukavu. Mshairi ameteua maneno yaliyosheheni sauti hizo za vipasuo ili kumpa msomaji picha ya ugumu unaotokea katika miktadha mbalimbali katika maisha. Maneno kama pigo, pigika, juto, shaka, komaa na usiku yanaashiria hali zisizovutia, yaani hali ngumu.

Mbali na Mashairi ya Saadani, mchango wa fonolojia katika kueleweka kwa ushairi unabainika katika diwani ya *Malenga wa Bara*. Katika diwani hiyo kwenye shairi liitwalo ‘Wimbo Kabla ya Kulala’ (uk.79), tunaona watunzi wanatumia sauti za vikwamizi ili kumithilisha hali ya wororo, ukimya, mvumo wa upepo, hisia za majuto, wivu, laana, woga, uchungu na kubezwa au kutwezwa. Kwa kuwa shairi hili ni la mapenzi, na kwamba, mashairi yanayohusu mapenzi mara nyingi yametajwa na wachambuzi mbalimbali kutumia sauti nyororo na laini (Magnus, 2013 na Blake, 2008), vikwamizi hivyo vinawasilisha vizuri suala hilo kama inavyobainika katika ubeti ufuatao:

Lala salama, e wangu mpenzi,  
Uote ndoto za tiba azizi  
Nina simanzi kukuaga mwenzi!  
**Hili ni wazi, walijua mwenzi!**  
Lala salama e wangu mpenzi  
Kesho salama, amka mwangazi.

Katika ubeti huu, vikwamizi katika maneno kama “salama,” “azizi,” “simanzi,” “mpenzi,” “mwenzi” na “mwangazi” ambavyo ni fonimu ‘s’ na ‘z’ vinaakisi hali ya wororo. Hizi ni sauti zinazogusa hisia za mapenzi, uzuri, heri, na majaliwa. Matumizi ya vikwamizi kuashiria hisia za mapenzi yalichunguzwa na mtafiti, pia katika utafiti wa uwandani katika sauti za watangazaji wa vituo mbalimbali vya redio jijini Dodoma. Vipindi vingi vinavyohusu masuala ya mapenzi ambavyo mara nyingi hurushwa kuanzia saa nne usiku katika redio hizo, sauti za watangazaji huwa na msikiko wa kipekee sana kutokana na matumizi ya vikwamizi. Vipindi hivyo ni kama vile *Usiku wa Wapendanao*, *Njozi Njema* na *Usiku wa Mahaba*. Kwa mfano, kuna kipindi kiitwacho ‘*Voice of Love*’ ambacho hurushwa hewani kuanzia saa nne hadi saa sita usiku. Kipindi hicho huwa hewani kuanzia siku ya Jumatatu hadi Alhamisi katika redio Dodoma FM inayopatikana katika masafa ya 98.4. Kipindi kingine kinaitwa *Anga za Mapenzi* na kinarushwa kuanzia saa tano usiku katika redio Kiss FM katika masafa ya 89.4. Pia, kipo kipindi kingine kinachoitwa ‘*Love Time*’ ambacho nacho hurushwa kuanzia saa tano usiku katika redio EFM, kwa Dodoma kipindi hiki kinapatikana katika masafa ya 92.5. Sauti ambazo hutumiwa zaidi ni sauti za vikwamizi hasa zile zenye sifa ya umuluzi, sauti kama /s, z, ʃ/. Sauti hizi zina sifa ya utulivu na ukimya, hazishitui bali hubembeleza na kuliwaza. Pia, humfanya mtu alale hata kama alikosa usingizi kwa sababu ya mawazo mengi.

Kwa jumla, sauti ni kiambajengo muhimu katika ushairi na hutegemea mahali sauti ilipo katika neno na katika mshororo. Sauti zina mchango katika uelewekaji wa ushairi, hali kadhalika katika uibuaji wa hisia katika ushairi. Mshairi huwa mtu makini, mwenye utulivu na mwenye majukumu kama ya fundi yeyote yule. Mshairi hupanga maneno huku akiwa makini katika uhusiano wa maana za maneno na hisia za sauti katika maneno hayo. Hali ya hisia anazozipata mshairi wakati wa utunzi hutarajiwa kumpata msomaji, ambaye hutumia akili na macho katika kuibua maana zinazoambatana na ujumi wa sauti kupitia hisia za sauti katika maneno ya ushairi. Ujumi wa ushairi umejikita hasa kwenye muumano uliopo kati ya maana, sauti na hisia. Mvuto wa sauti katika ushairi una umuhimu kama ilivyo maana ya ushairi wenyewe. Hata hivyo, sauti na maandishi havitengani, sauti ya maandishi humfikisha msomaji katika uga wa masikizi.

### **Mchango wa mpangilio na uradidi wa vina**

Mulokozi na Kahigi (1988) wanafafanua kuwa vina ni sauti za kufanana ambazo hurudiwarudiwa mwishoni, katikati ya mshororo au kila baada ya silabi kadhaa. Vina ni silabi zenye mpangilio fulani maalumu katika mshororo, ubeti, au shairi. Sanga na Philipo (2017) wanafasili silabi kuwa ni kipashio cha kifonolojia kinachohusu matamshi ambapo kwacho sauti za lugha hutamkwa mara moja kwa pamoja kama fungu au pigo moja la sauti. Katika lugha ya Kiswahili, silabi zaweza kuundwa kwa irabu moja, king'ong'o kimoja chenye usilabi na silabi zenye muunganiko wa konsonanti moja au zaidi na irabu. Aghalabu, maneno ya lugha nyingi hutamkwa kwa kufuata utaratibu wa silabi, ijapokuwa utamkaji wa silabi hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine. Hapa ieleweke kuwa dhana

inayoeleweka kama silabi katika fonolojia ndio hiyo inayohawilishwa kama kina au vina katika ushairi.

Mulokozi na Kahigi (whj) wanaeleza kuwa katika ushairi matumizi ya vina hudokeza hali ya shairi kama vile furaha, masikitiko, kebehi hata ucheshi. Wanaeleza kuwa vina vya aina hiyo hufungamana na hisia za mtunzi kuhusu jambo analolieleza, ambapo anakusudia wasomaji wake wazishiriki na ziwaathiri. Tahadhari inayodokezwa katika matumizi ya vina ni kwamba sharti vina hivyo vifungamane na maudhui ya shairi. Zaidi, vina visaidie kudhihirisha, kusisitiza na kudhibiti maudhui ya shairi.

Umuhimu wa vina katika ushairi huwa bayana pale tunapovihusisha na utamkaji wa sauti. Vina vinatusaidia kuchunguza mahusiano ya sauti katika shairi kuwa ni za kufanana au kutofautiana. Eneo mojawapo linalotudokezea ufundi wa mshairi katika upangaji wa maneno ni kupitia mpangilio wa vina. Kwa kuwa vina ni silabi zenye mlio wa kufanana, mashairi mengi ya ushairi wa Kiswahili wa kimapokeo huwa na vipande viwili: Kipande cha kwanza katika mshororo huitwa ukwapi na kipande cha pili katika mshororo huitwa utao. Vilevile, mshororo wa sauti wa shairi huweza kuwa na vipande vitatu, ambapo vina vya mwanzo huitwa ukwapi, vya kati ni utao na vya nje au mwisho huitwa mwandamizi kwa ushairi wenye vipande vitatu. Kwa jumla, katika shairi, vina huwa na dhima zifuatazo: Huongeza mvuto wa shairi, husisitiza maudhui, na hurahisisha kukariri shairi kichwani. Pia, marudiorudio ya sauti katika vina husaidia kujenga kumbukumbu ya maneno na maudhui ya utungo. Hali kadhalika, vina huchangia katika mpangilio wa kifonolojia na kisemantiki katika utungo wa ushairi (Sanga, 2014).

Tukirejelea mgogoro wa ushairi wa Kiswahili uliotokea miaka ya 1970 (Mayoka, 1986), hoja kuu ya wanamapokeo juu ya ushairi kwa wanausasa ilikuwa msisitizo wa vina na mizani kuwa uti wa mgongo wa ushairi wa Kiswahili. Ijapokuwa vina ni muhimu katika ushairi, msisitizo wa wanamapokeo ulizidi uhalisi, vina na mizani sio vipengele pekee vyenye umuhimu katika ushairi. Abeid (1954) anaeleza kuwa mawazo ya mtunzi yazue vina. Hii inaukilia kuwa ndani ya urudiajirudaji wa vina kumebebwa msisitizo juu ya maana au maudhui ya shairi. Kwa mfano, katika shairi la ‘Tumlilie Mdanzi’ katika kitabu cha *Mashairi ya Saadani* (uk. 53) ubeti wa 11 mwandishi anasema:

Tumlilie Mdanzi, Razzaku hana hiyana,  
Dunia sio makazi, viumbe kutulizana’  
Hata kina sisimizi, kufa ni lazima sana,  
Bilali Mshoro bwana, tumlilie Mdanzi

Marudio ya vina yanayojitokeza katika shairi hili ni kina cha ndani ‘zi’ na kina cha nje ‘na’. Vina hivi vimetumiwa ili kuisisitiza na kuwakumbusha waja juu ya kifo. Mwandishi ametumia kina cha ‘zi’ kudhihirisha hisia za majonzi aliyonayo juu ya mpendwa wake, msanii mwenzake Mdanzi. Pia kina cha ‘na’ kinasisitiza juu ya uwapo wa kifo, kwamba ni jambo lisiloepukika. Suala la kina cha ‘zi’ hapa kudhihirisha hisia za majonzi ni la kidhana zaidi na limejengwa kutokana na uzoefu wa msomaji kuhusu hisia zibebwazo na sauti katika mazingira yake kijamii. Hili linashadidiwa na mawazo ya wananadharia ya umuundo katika isimu ya lugha kuwa lugha ina pande mbili: Kitaja na kitajwa. Kitaja ndicho kimebeba dhana na ndicho huibua hisia zihusianazo na kitajwa (Sturrock, 1979 na Scholes, 2009). Kina cha ‘na’ kinasisitiza ujumbe wa kifo kwa kuwa maneno kama Razzaku, viumbe na kufa yanawekewa kishindo na silabi hiyo ya ‘na’.

Nao Mulokozi na Kahigi (whj) katika *Malenga wa Bara* wameonesha ufundi wao katika kudhihirisha na kusesitiza maudhui ya shairi kwa marudiorudio ya vina, yaani silabi kwa misingi ya fonolojia. Katika shairi la ‘Kitu Nisichokitaka’ (uk. 10) ubeti wa kwanza na wa tatu waandishi wanasema:

Kitu nisichokitaka, ni nguo yenye kiraka,  
Ingawa kinafunika, pale palipotatuka,  
Na pengine hutumika, hata zaidi ya mwaka,  
Mimi sitaki kiraka, nguoni kukipachika.

Siyo kwamba ninacheka, hata! Nimekasirika!  
Kama nisipoehuka, Sitakivaa kiraka!  
Heri nguo kuiweka, kwenye jalala la taka,  
Kuliko kuvaa kiraka, kuliko kuvaa kiraka!

Kiraka ni kipande cha nguo ambacho hushonewa kwenye nguo, hasa iliyochakaa kiasi cha kuacha uwazi ambao unaonesha mwili wa aliyevaa. Aghalabu, kwa wanaume nguo kama suruali huanza kuchakaa kwenye makalio na magoti. Kiraka hakitumiki kwenye nguo pekee, bali hutumiwa pia kwenye vitu vingine kama vile matairi ya magari yaliyotoboka. Kina cha ‘ka’ kimerudiwarudiwa makusudi kwa lengo la kudhihirisha hisia za mshangao juu ya tabia za kiraka. Aidha, waandishi wametumia kina hiki cha ‘ka’ kama msisitizo katika kupinga maisha bandia kama vile kupaka dawa ya piko kwenye mvi ili nywele ziwe nyeusi kuficha uzee. Ufafanuzi huu umejigeza katika mawazo ya wanamuundo kuwa maana katika kazi ya fasihi hupatikana kutokana na mahusiano ya vipengele vya kimuundo ndani ya kazi yenyewe (Sturrock, khj na Scholes, khj).

Silabi (vina) ndicho kipimo cha msingi katika upangaji wa utaratibu wa matamshi wa lugha. Tumekwishafafanua hapo juu kuwa msingi wa ushairi upo katika umbo sauti ambamo ndimo zimebebwa hisia za mtunzi. Vina ni

kipashio cha kisauti, maana ya shairi itaeleweka kwa urahisi ikiwa uamilifu wa vina katika shairi unafahamika. Obermeler na wenzake (2016) wanashadidia kuwa matumizi ya vina na mpangilio maalumu wa mizani katika ushairi husaidia kuongeza ubora wa kiujumi, msikiko au msisitizo, ukubalifu, na hisia.

### **Mchango wa wizani**

Stickney (1840) anaeleza kuwa, katika masomo yote, sauti ndiyo ina muunganiko wa karibu na hisia za ushairi. Hili linachangiwa na kigezo cha kueleweka ndani ya uga mpana kutokana na ushawishi wa kimuziki, nguvu ya uzuri na asili ya hisia. Pia, ndani ya ushairi kuna mpangilio wa mapigo (wizani) unaotambulika kwa watumiaji wa lugha husika. Mulokozi na Kahigi (whj) wanafafanua zaidi kuhusu wizani au ridhimu kuwa ni mapigo asilia ya lugha. Kila lugha ina mapigo na mawimbi yake ya sauti yenye kupanda na kushuka, na yanayofungamana na maana. Wizani wa ushairi na muziki hutokana na vipindi vya mapigo ya lugha au sauti. Asili ya wizani wa kishairi ni wizani asilia uliomo katika maumbile, mazingira na shughuli za binadamu. Hivyo, wizani wa ushairi hulazimika ulandane na maudhui ya shairi hilo ili usaidie kuyadhihirisha maudhui hayo kihisia, kimtiririko na kimsisitizo.

Wananadharia walioshughulikia masuala ya uchambuzi wa kazi za sanaa kwa kurejelea hisia za mtunzi wanakubaliana kuwa kuna mshabihiano bayana kati ya sifa za kazi ya sanaa na hali ya hisia za msomaji. Msomaji atapata hisia katika shairi ikiwa: Kazi X (kwa mfano shairi) itaonekana kuibua hisia Y (hali ya hisia) kama tu kuna ushabihiano kati ya X na Y (Langer, 1953 na Goodman, 1976). Kwa mintarafu hii, kuna uwezekano mkubwa kuwa msomaji mmoja anaweza kusoma shairi asipatwe na



msisimko wowote na mwingine akalिसoma shairi hilohilo akajawa na hisia kama za huzuni au furaha. Aghalabu, wimbo wenye wizani wa polepole huashiria huzuni na ule wa harakaharaka huashiria furaha. Watu wanapokuwa katika matukio yanayotia majonzi kama vile msiba, huwa hawaoneshi uchangamfu wowote. Kunakuwa na sauti za chini, matendo ya polepole na hali fulani za wororo. Kwa jumla, uharaka na uchangamfu hukosekana, lakini kwenye matukio ya furaha kama vile katika sherehe za harusi, watu huchangamka na nyimbo huwa ni za harakaharaka. Hivyo, sifa hizo zitashabihiana na wimbo au ushairi wa polepole au harakaharaka. Izingatiwe kuwa sifa hizo tunazozieleza hazimhusu msanii ila kazi ya sanaa yenyewe, bila kuzingatia hali ya hisia alizokuwa nazo mtunzi wakati wa utunzi kwamba ni za furaha ama huzuni (Sanga, 2018). Ikumbuke kuwa Nadharia ya Umuundo tuliyoigusia hapo juu inaeleza kuwa, ili kazi fulani ya sanaa ionekane inagusa hisia za msomaji, haipingiki kuwa kuna sifa zinazoshabihiana kati ya kazi ya sanaa na mtu. Nadharia hiyo inasisitiza zaidi kuwa mahusiano ya vipengele katika kazi za fasihi ndiyo hutupatia maana.

Maelezo hayo yanathibitika katika mashairi teule. Kandoro (1972), katika *Mashairi ya Saadani*, anarejelea mazingira, shughuli na matukio kwa kutumia mapigo ya sauti. Kwa mfano, katika ubeti wa 7 wa shairi la ‘Tumshukuru Manani’ uk. 147 inaelezwa:

Leo nasi twajaliwa, tuwe huru duniani.  
Tuondokwe na ukiwa, tuwe viumbe thamani,  
Tupate kuthaminiwa, baraza ya duniani,  
Tunamshukuru manani, uhuru tumejaliwa.

Shairi hili lina mapigo ya mwendo wa haraka. Kwa mujibu wa Langer (khj) na Goodman (khj), mshairi anatuonesha hisia zake za furaha juu la tukio la

Tanganyika kupewa uhuru wake kutoka kwa wakoloni Waingereza. Kandoro anataeleza mwenyewe katika kitabu hiki kuwa yeye ni miongoni mwa wanajeshi waliopigania uhuru. Pia, alikuwa miongoni mwa wanachama 17 waanzilishi wa chama cha TANU. Hivyo, shairi hili la ‘Tumshukuru Manani’ lilitumika kuelezea hisia za furaha aliyokuwa nayo juu ya kupatikana kwa uhuru. Hili ni shairi linalosherehekea uhuru. Mukadha wa yale anayoyasimulia marehemu Kandoro ndio unatuongoza kwenye mapigo ya shairi hili. Mwandishi anasimulia majaliwa ya mtu aliyekuwa kifungoni na akaachiwa huru, ameondokana na ukiwa na uduni akawa mtu mwenye thamani duniani. Hapa tunapata taswira ya hisia za mtu anayesimulia jambo kwa vitendo mithili ya mtu anayeeleza jambo kwa shangwe. Hivyo, wizani wa shairi hili unakwenda sambamba na maudhui ya shangwe.

Kipengele hiki cha wizani kipo bayana pia katika mashairi huru, yaani mashairi ya wanausasa. Katika diwani ya *Malenga wa Bara* (kur. 15 - 16) kuna shairi la ‘Maombolezo ya Mtu Maskini’. Katika shairi hili, waandishi wanaeleza jitihada za mtu maskini au mnyonge zinavyokwamishwa na mifumo inayomtawala. Masimulizi ya shairi hili ni ya kitanzia. Kwa mfano, katika ubeti wa nne waandishi wanasema:

Nimekuwa mtumwa katika dunia huru  
Fakiri katika jumuiya tajiri;  
Nachungwa na kuswagwaswagwa  
Kama sarakasi katika uzi!  
Kwa nini? Najiuliza.  
Kwa nini nasumbuka hivi, kwa nini nateseka hivi?  
Natangatanga, nadidimia, nageuka kiguu na njia?  
Sijui.  
Labda nilikufa kabla ya kuzaliwa,  
Na sasa naishi baada ya kufa.  
Katika enzi zizokuwa zangu,

Katika nchi isiyokuwa yangu  
Labda siishi ila nipo tu  
Kama kitu tu, kama kijiwe tu, kama kijiti tu!  
Labda haipo siku ya wokovu abadan!

Shairi hili linaweka bayana madhila mbalimbali wanayowapata tabaka la wanyonge. Kila wanapofanya jitihada za kujikwamua na unyonge wao, hali inarudi kuwa vilevile. Tukirejelea ufafanuzi wa hapo juu masimulizi ya mtu masikini ni ya wizani usio na mapigo ya haraka. Zaidi, ni mapigo yanayosawiri mtu aliyejawa na mawazo, anayejiuliza katika nafsi yake kwamba hali aliyonayo itakwisha lini? Mtu masikini anajifananisha na msukule, kwamba labda alishakufa na sasa anaishi katika enzi ambazo sio zake, labda yeye ni kama kitu au kijiwe au kijiti. Katika shairi hili, kuna kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti kunakoakisi hali ya kutangatanga, kwenda mbele kisha kurudi tena palepale. Kadri waandishi wanavyosimulia mazingira ya mtu masikini ya kuwaza na kuwazua kuhusu hali yake, vivyo ndivyo mapigo ya shairi hili yanavyokwenda sambamba na hali hiyo. Kwa jumla, wizani wa ushairi unafungamana na mazingira ya binadamu. Wizani una mchango katika kuuelewa ushairi kwa kuwa unasaidia kudhihirisha maudhui ya shairi kihisia, kimtiririko na kimsisitizo.

### **Mchango wa mkazo**

Sanga na Philipo (2017) wanafafanua kuwa mkazo ni sifa ya kiarudhi katika matamshi. Hii ni sifa ambayo haihusiki na fonimu irabu wala konsonanti pekee bali ni ya silabi. Mkazo ni hali ya silabi katika neno kusikika kuwa na nguvu zaidi kuliko silabi nyingine katika neno. Silabi inayotamkwa kwa mkazo ina msikiko mkubwa zaidi kuliko silabi nyingine katika matamshi ya neno hilohilo. Sio lugha zote duniani hutumia mkazo, zingine, kama vile lugha nyingi za Kibantu, isipokuwa Kiswahili, hutumia toni badala ya

mkazo. Attridge (1982) anafafanua kuwa mkazo ni matokeo ya utangamano wa mambo kadhaa, yakiwamo urefu wa silabi, kidatu, sifa ya irabu na msikiko. Anaeleza kuwa, mara nyingi, inafahamika kuwa silabi yenye mkazo ndiyo husikika zaidi, lakini ukweli wa kimaabara unaonesha kuwa silabi zenye mkazo ni laini na nyororo kuliko nyingine. Anasisitiza kuwa utambuzi wa mkazo upo katika maarifa ya mtumia lugha anayejua muundo wa lugha husika kuliko elimu ya kiakustika.

Zipa lugha kama vile Kiingereza na Kijerumani ambazo matumizi ya mkazo ni makubwa kiasi kwamba hayatabiriki. Pia, kuna lugha kama vile Kicheki, Kiswahili na Kipolishi ambazo mkazo hutabirika. Katika Kiswahili, mkazo huwekwa katika silabi ya pili kutoka mwishoni mwa neno (Sanga na Philipo, whj).

Katika utafiti wetu, tumebaini kuwa matumizi ya mkazo katika ushairi yana dhima mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kusababisha lugha zitofautiane wizani na kuongeza wakaa wa silabi yenye mkazo katika utamkaji. Katika shairi la ‘Siafu Wamekazana’ (uk.138) katika *Mashairi ya Saadani*, silabi zilizokozwa ndizo huwekwa mkazo wakati wa kusoma au kughani shairi husika. Mkazo huo una dhima kubwa katika uelewekaji wa shairi husika kama inavyobainika katika ubeti wa kwanza ufuatao:

**Nyoka amegutuka, ndani ya shimo katuna,**  
**Tena amekasirika, hasira zenye kununa,**  
**Nyoka anababaika, shimoni kwa kujikuna,**  
**Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.**

Kutokana na mkazo uliowekwa kwenye silabi zilizokozwa kwenye shairi hilo, msomaji wa shairi hilo hupata wepesi wa kulielewa. Msomaji anajulishwa kuwa maneno yenye mkazo ndiyo hasa yenye umuhimu katika

ushairi, na kwamba, mengine yaliyopo ni ya ziada ili kukamilisha utungo au kujaliza mshororo.

Mkazo una dhima ya kuweka msisitizo juu ya jambo lililokusudiwa kuwasilishwa kupitia silabi katika maneno au kupitia maneno katika sentensi. Pia, mkazo una dhima ya kutofautisha maana katika usemi, hasa katika tungo zenye maana zaidi ya moja. Katika *Malenga wa Bara*, shairi la ‘Sima na Mayai’ (uk. 71) ubeti wa sita, mkazo unajitokeza katika sentensi na kumsaidia msomaji kubaini maana ya utungo, tumekoza yenye mkazo kama ifuatavyo:

**Kikumbuke**  
Kibwebwe chako **nilichokushonea**  
**Likumbuke** shati lako la kaniki  
**Likumbuke** kaptura lako la kaki  
**Zikumbuke** talawanda **nilizokushonea;**  
Na **ulipokwenda** shule  
Masafa ya kilometa kumi  
**Zilikusetiri** katika changarawe

Ushairi ni utungo unaotumia lugha ya mkato. Mshairi huteua maneno machache, hasa yale aliyokusudia yafikishe ujumbe. Katika matumizi ya lugha ya kawaida, ni vigumu kumwelewa mtu anayeongelea jambo kwa mkato. Aghalabu, huwa inahitajika pawe na ufafanuzi wa kina ili ujumbe wake ueleweke. Katika mintarafu ya lugha hiyo ya ushairi, mkazo unakuwa kipengele kimojawapo kinachosaidia kubaini maana iliyokusudiwa na mtunzi wa shairi. Shairi la ‘Sima na Mayai’ linamtaka msomaji akumbuke maisha yake ya awali aliyoyishi na wazazi wake kijijini. Waandishi wanamkumbusha msomaji asisahau waliomfikisha hapo alipo. Msisitizo wa shairi ni kurejelea katika siku za nyuma; hivyo, mkazo unawekwa kwenye maneno yanayorejelea wakati uliopita. Vitenzi kama vile *kikumbuke*,

*nilichokushonea, likumbuke, zikumbuke, nilizokushonea, ulipokwenda* na *zilikusetiri* katika ubeti huu vinawekewa mkazo kuliko maneno mengine kwa kuwa msisitizo wa utungo ni kukumbusha. Ieleweke kuwa wazawa au watumiaji wa lugha wana uwezo wa kuubaini kwa wepesi mkazo katika tungo za lugha yao na dhima iliyokusudiwa na msemaji.

### **Mchango wa kiimbo**

Kiimbo ni sifa ya kiprosodi katika lugha. Kiimbo kinahusu hali ya mpandoshuko wa mawimbi ya sauti ya lugha. Kila lugha ina utaratibu maalumu wa kupanda na kushuka kwa sauti zake. Kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti husaidia kubainisha lengo la usemaji lililokusudiwa na mzungumzaji wa lugha husika. Kiimbo hutusaidia kujua iwapo mzungumzaji anatoa maelezo, anaamrisha, anahoji au anauliza swali au anastaajabu (Sanga na Philipo, 2017).

Kiimbo huwa bayana zaidi katika ushairi simulizi kuliko ushairi andishi. Ijapokuwa msomaji wa ushairi hupungukiwa na hali ya umuziki iliyomo katika sauti za maneno, bado upo muunganiko wa karibu sana wa sauti na maandishi. Maarifa ya kutusha sauti ya kuhoji, kushangaa, kuuliza au kueleza katika mshororo yapo akilini mwa mtumia lugha. Wizani, mpangilio wa vina, mpangilio wa sauti katika maneno pamoja na tukio ambalo mtunzi analisimulia, vina mchango wa kuelekeza mahali pa kupandisha au kushusha sauti ili kuendana na maudhui ya ushairi. Mfano wa kiimbo kinavyonaweza kutushwa unapatikana katika shairi liitwalo ‘Kwetu ni Kwao Kwa nini?’ (uk.139) katika *Mashairi ya Saadani*. Hapa tumerejeelee ubeti wa tatu na wa nne:

Kwa nini kwao kwa nini, kuwe kwetu ni kwa nini?  
Na kwetu pia kwa nini, kuitwa kwao kwa nini?  
Kwa nini inayakini, kwetu ni kwao kwa nini?

Kwetu ni kwao kwa nini, na kwao kwetu kwa nini?

Mtu kwao kuthamini, ijapokuwa jiweni,

Pia alale mtini, na baraza liwe chini,

Nile matunda porini, kuitwa kwenu kwa nini?

Kwetu ni kwao kwa nini, na kwao kwetu kwa nini?

Msomaji wa beti za shairi hili atatumia kidatu kulingana na maudhui ya shairi. Katika mishororo ya ubeti wa tatu, kitatumika kiimbo cha swali, ambapo kidatu huwa katika mstari ulioinuka. Hapo, mwandishi anauliza sababu za wakoloni kutawala nchi zetu za Afrika, vigezo gani wametumia kuhlalisha na kuzichukulia nchi za Afrika kama miliki zao. Kidatu kinachotumika hapa ni cha kupanda. Kiimbo kitakachotumika katika mshororo wa kwanza na wa pili wa ubeti wa nne ni cha maelezo. Sauti ya msomaji inakuwa katika mstari ulionyooka. Mwandishi anatoa ufafanuzi juu ya mtu kuridhika na chake, na akithamini kwa kuwa chake, pasipo kujali wengine wanakionaje. Katika mishororo miwili ya mwisho katika ubeti wa nne mwandishi anapandisha tena kiimbo akihoji kuwa hata kama ninaishi maisha yangu ni duni, ninaishi kwa kula matunda, sipaswi kupokwa kwetu.

### **Hitimisho**

Hakuna kanuni za jumla za kiisimu katika ushairi kwa lugha zote. Kila ushairi hutumia kanuni za kiisimu zinazoendana na lugha husika. Hatuwezi kupuuza mwingiliano, kuathiriana na kutegemeana kwa vipengele vya kiisimu na lugha ya ushairi (fasihi). Haikanushiki kuwa mtunzi wa ushairi ana idhini ya kishairi ambayo inampa uhuru wa kufanya ukiushi wa kifonolojia, kisemantiki, kisintaksia, kitahajia, kisarufi na kileksikografia (Leech, 1969). Pamoja na uhuru huo, bado mtunzi na msomaji wanalazimika kuzingatia kanuni za kiisimu kwa sababu lugha ya kifasihi

haiwezi kuwapo pasipo lugha ya kawaida. Hivyo, ili kuulewa ushairi na maudhui yake, hatuna budi kuzingatia vipengele vya kiisimu, vikiwamo vya kifonolojia. Vipengele vya kiisimu ni viungo muhimu katika ujifunzaji wa ushairi, hasa tukianza na hivi vya kifonolojia ambavyo ni: Mpangilio na uradidi wa fonimu, mpangilio na uradidi wa silabi (vina), wizani, kiimbo na mkazo, hivi ni vya msingi kwa kuwa msingi wa lugha ni sauti. Mtunzi na msomaji wa ushairi wanapaswa kuzielewa dhana na alama mbalimbali za kiisimu.

### **Marejeleo**

- Abeid, A. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: EALB.
- Attridge, D. (1982). Poetic Meter, Literary Criticism, Linguistic Rhythm, Reading, Lexical Stress, Sentence Stress, Syllables. *Poetics Today*, 17(1), 51 - 54.
- Bahadorj, S. na Mohammadjalil, A. (2012). Role and Function of Sound (phonemes) in Persian Language, by Analysis of Hafez Poems. *Literary Aesthetics of Azad University*, 5(17), 87 - 114.
- Barry, J. na Blake, B. J. (2008). *All about Language*. London: Oxford University Press.
- Culler, J. (1975). *Structuralist Poetics: Structuralism, Linguistics and the Study of Literature*. Ithaca, N.Y: Cornell University.
- Goodman, N. (1976). *Language of Art: An Approach to a Theory of Symbols*. Indianapolis: Hackett.
- Kahigi, K.K. na Mulokozi, M.M. (1976). *Malenga wa Bara*. Dar es Salaam: EALB.
- Kandoro, S.A. (1972). *Mashairi ya Saadani*. Dar es Salaam: Mwananchi Publishing Ltd.



- Langer, S. K. (1953). *Feeling and Art: A Theory of Art Develop from Philosophy in a New Key*. New York: Charles Scribner's Sons.
- Leech, G. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman.
- Magnus, M. (2013). A History of Sound Symbolism. In K. Allan (Ed.), *The Oxford Handbook of the History of Linguistics* (pp. 93 - 115) London: Oxford University Press.
- Massamba, D. P. B. (2010). *Phonological Theory: History and Development*. Dar es Salaam: DUP.
- Mayoka, J. (1986). *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka*: Dar es Salaam: T.P.H.
- Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuu Vikuu*. Dar es Salaam: KAUTTU Ltd.
- Njogu, K. na Chimerah R. (2008). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Samwel, M. (2012). *Hadithi Fupi: Nadharia, Mbinu na Mifano*. Iringa: Kasenyenda Tanzania.
- Sanga, A.N. na Philipo, T.P. (2017). *Fonolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Karljamer Publishers Ltd.
- Selden, R. (1989). *A Reader's Guide to Contemporary Literary Theory*. New York: Harvester Wheatsheaf.
- Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi: Mfululizo wa Lugha na Fasihi, Kitabu cha Kwanza*. Dar es Salaam: KAUTTU Ltd.
- Scholes, R. (2009). *Structuralism in Literature: An Introduction*. New Haven: Yale University Press.

A.N. Sanga

- Senkoro, F. E. M. K. (1988). *Ushairi: Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Stickney, S. E. (1840). *The Sons of the Soil*. Iliyosomwa katika <http://www.indiana.edu/~letrs/vwwp/ellis/sons.html>
- Sturrock, J. (1979). *Structuralism and Since: From Levi Strauss to Derrida*. Oxford: Oxford University Press.
- Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers Ltd.
- Wamitila, K. W. (2004). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: English Press.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.